TANGAZO LA SERIKALI NA ........ la tarehe ..../..../2024

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

(SURA 290)

# SHERIA NDOGO

Zimetungwa chini ya Kifungu vya 7(1) na 16 (1)

SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA STENDI NA MAGARI) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YASERENGETI ZA MWAKA, 2024

Jina na mwanzowa kuanza kutumika

Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ushuru wa Stendi) za Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti za mwaka, 2024 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo-

"*Afisa Mwidhiniwa*" maana yake ni Afisa ye yote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"Bajaji" maana yake ni pikipiki yo yote ya magurudumu matatu;

"*Chombo cha usafiri*" maana yake ni chombo cho chote cha moto, Gari, Pikipiki ya magurudumu mawili au matatu;

"*Halmashauri*" maana yake Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti;

“*Kituo cha basi*” maana yake ni eneo maalum lililotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kutolea huduma za usafiri ambapo mabasi au vyombo vingine vya usafirishaji wa abiria vitapakia au kushusha abiria na mizigo yao;

“Maegesho” maana yake ni sehemu

iliyoainishwa na Halmashauri kwa ajili ya kuegesha chombo cha usafiri isipokuwa stendi;

"Maegesho maalum" maana yake ni eneo maalum lililotegwa na Halmashauri kwa ajili ya kuegesha vyombo vya usafiri vilivyokamatwa kwa makosa mbalimbali;

"*Mkurugenzi*" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti pamoja na Afisa ye yote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"*Ushuru wa Stendi* " maana yake ni ushuru unaotozwa na Halmashauri kwa mtu ye yote anayeingia na chombo cha usafiri katika eneo la stendi;

"Yadi" maana yake ni eneo maalum lililotengwa kwaajili ya kuhifadhi vyombo vya usafiri;

Eneo la Stendi

(1) Halmashauri itatenga eneo la stendi kwa ajili ya kupakia au kushusha abiria ndani ya Wilaya ya Serengeti.

(2) Itakuwa ni wajibu kwa mtu ye yote anayefanya biashara ya kusafirisha abiria, kupakia au kushusha abiria katika eneo la stendi tu;

(3) Gari la abiria au mizigo litaruhusiwa kupakia au kushusha mzigo katika eneo la stendi kuanzia saa kumi na mbili (12:00) asubuhi mpaka saa nne (4:00) usiku;

(4) Kila Gari la abiria linaloingia katika eneo la stendi litakuwa na kibao au maandishi yanayoonesha mahali

la abiria itaanzia kwenye stendi isipokua kwa gari inayopita kutoka maeneo mengine ya nje ya Halmashauri;

yaAfisa Mwidhiniwa

(6)

Ushuru waStendi

Wajibu wa kulipa Ushuruwa Stendi

Namna ya kutoza Ushuruwa Stendi

Mamlaka

Garilaabiriahalitaruhusiwakusimamakwazaidiyad

akika tano katika kituo cha njiani baada ya kuanza safari kutoka eneo la stendi;

(7) Gari la abiria au mizigo litaruhusiwa kukaa katika eneo la stendi kwa muda usiozidi masaa mawili;

(8) Halmashauri itatenga eneo maalum ndani ya eneo la stendi kwa ajili ya kupakia au kushusha mizigo;

(9) Bila kuathiri masharti ya kifungu 4(3) cha Sheria Ndogo hizi, gari la abiria au mizigo linaweza kupakia au kushusha mizigo kabla ya saa kumi na mbili (12:00) asubuhi na baada ya saa nne (4:00) usiku kwakibali cha Halmashauri.

5. Halmashauri itatoza Ushuru wa Stendi kwa mujibu wa viwango vilivyoanishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi.

6. (1) Itakuwa ni wajibu kwa mtu ye yote anayekusudia kupakia au kushusha abiria au mzigo katika eneo la stendi kulipa ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu cha 6(1) cha Sheria Ndogo hizi,itakuwa ni wajibu wa kila mfanyabiashara wa chombo cha usafiri kuhakikisha kwamba chombo chake kimesajiliwa na Halmashauri na kupewa namba ya usajili kabla ya kuanza biashara, viwango vya usajili ni kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi.

7. (1) Ushuru wa stendi utalipwa na mtu ye yote anayekusudia kupakia au kushusha abiria mara tu anapoingia katika eneo la stendi; au kwa mwezi kadriHalmashauri itakavyoona inafaa;

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu cha 5(2) cha Sheria Ndogo hizi, chombo cha usafiri kinachomilikliwa na Serikali, Wanadiplomasia, na Majeshi na taasisi za dini hakitatozwa ushuru wa stendi.

8. (1) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na mamlaka ya kukamata na kuondoa chombo cha usafiri

a
m
b
a
c
h
o
k
i
t
a
p
a
k
i
a
a
u

kushusha abiria nje ya stendi au eneo lisiloruhusiwa, au hakijalipiwa ushuru wa stendi au hakijasajiliwa kwa mujibu Sheria Ndogo hizi;

(2) Chombo cha usafiri kilichokamatwa kwa mujibu wa kifungu cha 8(1) kitaondolewa na kuhifadhiwa katika Yadi ya Halmashauri au sehemu yoyote iliyoainishwana Halmashauri;

(3) Baada ya kuomba na kupata kibali cha Mahakama Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuuza chombo cha usafiri endapo mmiliki wa chombo atashindwa kulipa gharama za kukiondoa ndani ya siku 14 tangu tarehe ya kukamatwa.

Makosa

9. Mtu ye yote atakuwa ametenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi ikiwa:-

(1) atashindwa kulipa ushuru wa stendi;

(2) atamshawishi mtu ye yote au kundi la watu kutolipa ushuru wa stendi;

(3) atapakia au atashusha abiria katika eneo ambalo siyo stendi;

(4) atapiga debe katika eneo la stendi;

(5) atafanya matengenezo au kuosha gari katika eneo la stendi;

(6) gari lake la abiria au mizigo litaendelea kuwepo katika eneo la stendi zaidi ya masaa mawili;

(7) atalaza gari lake au chombo kingine cha usafiri katikaeneo la stendi;

(8) atauza vyakula au vinywaji kwenye eneo la maegesho au stendi kinyume na utaratibu utakaoweka naHalmashauri;

(9) atapakia au kushusha mzigo nje ya eneo lililopangwa au kinyume na utaratibu ulioainishwa na Halmashuri

Adhabu. 10. Mtu ye yote atakayekwenda kinyume na masharti ya

Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi laki mbili (200,000/=) na isiyozidi shillingi milioni moja (1,000,000) au kifungo kisichopungua miezi kumi na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote kwa pamoja faini na kifungo.

Kufifilisha kosa

11. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza faini ya kiasi kisichopungua laki mbili (200,000/=) na kisichozidi laki tano (500,000/=)mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi na kukiri kwa maandishi kwa kujaza fomu maalum iliyoambatanishwa kwenye Jedwali la Tatu la Sheria Ndogo hizi na atatakiwa kulipa ushuru wa stendi anaodaiwa.

JEDWALI LA KWANZA

(Limetungwa chini ya kifungu cha

5)USHURU WA STENDI

*(Ushuru wa Stendi)*

**USHURU WA MAGARI NA MIZIGO**

| ***Na.*** | ***Aina ya Gari*** | ***Kiasi cha ushuru*** | ***Muda*** |
|---|---|---|---|
| 1. | Mabasi makubwa | 5000 | Kila linapoingia stendi |
| 2. | Mabasi ya kati | 4000 | Kila linapoingia stendi |
| 3. | Magari madogo | 3000 | Kila linapoingia stendi |
| 4. | Taxi,Pick up, Kirikuu, bajaji, Ukiegesha ndani ya kituo cha basi | 2000 | Kwa saa |
| 5. | Taxi,Pick up, Kirikuu, bajaji, Ukiegesha ndani ya kituo cha basi | 5000 | Kwa siku |
| 6. | Pikipiki ikiegesha ndani ya kituo | 2000 | Kwa siku |
| 7. | Gari binafsi akiingia/ akiegesha nje na ndani ya kituo | 1000 | Kwa siku |
| 8. | Taxi,Pick up, Kirikuu, bajaji | 1000 | Kila linapoingia ndani ya kituo cha magari kushusha abiria na kutoka |
| 9. | Pikipiki | 200 | Kila linapoingia ndani ya kituo cha magari kushusha abiria na kutoka |

JEDWALI LA PILI

ADA YA USAJILI

Limetungwa chini ya kifungu cha 6(2)

| Na | Aina ya Chombo cha usafiri | Muda | Idadi | Kiasi |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Pikipiki | Kwa mwaka | Mara 1 | 15,000 |
| 2 | Bajaji | Kwa mwaka | Mara 1 | 15,000 |
| 3 | Teksi | Kwa mwaka | Mara 1 | 20,000 |

FOMU YA KUFIFILISHA KOSA
(Chini ya kifungu cha 11 cha Sheria Ndogo hizi)

Mimi…………………………………………wa S.L.P……………………… ninaefanya biashara ya ………………………………. katika eneo la………………………………lililopo ndani ya Halmashauri ya
Wilaya ya Serengeti.Nakiri kuwa leo tarehe………………………………nilikiuka masharti ya Sheria Ndogo za (Ushuru wa Maegesho) za Halmashauri ya Serengeti za Mwaka, 2024. Kwa hiyo, kwa hiari yangu mwenyewe na bila kushawishiwa na mtu yeyote, nakubali kulipa faini iliyoainishwakwenye Sheria Ndogo hizi iwapo Mkurugenzi atatekeleza madaraka aliyopewa chini ya kifungu cha 11 cha Sheria Ndogo hizi.

Saini ………………………………………………

Jina……………………………………………….

Tarehe …………………………………………….

Mbele yangu ……………………………………...

Saini ……………………………………………….

Wadhifa …………………………………….....

Tarehe …………………………………………….

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti imebandikwa kwenye Sheria Ndogohizi
kufutia Azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika mnamo tarehe………………………mbele ya :-

……………………………………

MAULID MADENI (PhD)
*Mkurugenzi Halmashauri ya Wilaya Serengeti*

L.S

……………………..
AYOUB M. MAKURUMA
*Mwenyekiti Halmashauri ya Wilaya Serengeti*